
# KISWAHILI NA UTAIFA NCHINI KENYA



Chama cha Kiswahili cha Taifa [CHAKITA]

Kimechapishwa na:

Twaweza Communications
Jumba la Twaweza, Barabara ya Parklands
Mpesi Lane
S.L.P. 66872 - 00800
Nairobi, Kenya
Simu: +(254) 020 375 2009; 020 269 4409
Barua pepe: info@twawezacommunications.org
Wavuti: www.twawezacommunications.org

© Haki ya kunakili ni ya Twaweza Communications na CHAKITA-Kenya

Chapa ya kwanza 2012

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kupiga chapa, kutafsiri
idhini ya Twaweza Communications na CHAKITA-Kenya.

**ISBN 978 9966 028 36 5**

Kimeruwazwa na Catherine Bosire
Jalada limesanifiwa na Apex Books & Publishers Ltd.

**SEHEMU YA PILI: Kiswahili katika Elimu**

Utetezi wa Elimu ya Uwililugha Afrika Mashariki ---------------------- 8
*Peter Githinji*

Mitaala ya Kiswahili katika Elimu na Utaifa: Nafasi ya Fasihi ya Watoto katika Utendelezaji na Uimarishaji wa Utaifa---------------- 10
*Pamela Muhadia Ngugi*

Ukiushi kama Mbinu ya Kudhihirisha Itikadi ya Kuumeni katika Fasihi ya Kiswahili: Mifano kutoka Riwaya za Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi ---------------------- 12
*Miriam Osore na Charlotte Ryanga*

ACALAN: Chombo Madhubuti na Asasi-Mlezi wa Lugha za Afrika ---------------------------------------- 13
*Naomi L. Shitemi*

Kiswahili na Umataifa -------------------------------------------------------- 14
*Anna M. Kishe*

Utandawazi na Ufundishaji wa Fasihi ya Kiswahili ------------------ 161
*Steven Elisamia Mrikaria*

Utatuzi wa Migogoro ya Kisiasa: Mafunzo ya Waswahili ------------ 181
*Mwanakombo Mohamed Hassan*

Waandishi wa Makala ------------------------------------------------------ 191

# UKIUSHI KAMA MBINU YA KUDHIHIRISHA ITIKADI YA KUUMENI KATIKA FASIHI YA KISWAHILI: MIFANO KUTOKA RIWAYA ZA SAID AHMED MOHAMED NA EUPHRASE KEZILAHABI

Miriam Osore na Charlotte Ryanga

## Utangulizi

Dhana ya ukiushi (defamiliarization) ina maana ya kudhihirisha kitu au hali kwa njia isiyokuwa ya kawaida, au isiyo dhahiri. Dhana hii hutumiwa kueleza kijumla hali ambapo kitu fulani hudhihirishwa kwa njia isiyo kuwa ya kawaida. Stacy (1977:178) anaeleza kwamba mbinu ya ukiushi inaweza kutumiwa kwa malengo mbalimbali; kama kuchekesha, kushangaza, kuhuzunisha, kukasirisha au kumfanyia mtu mzaha. Hata hivyo, mbinu hii imetumiwa kueleza uvumbuzi mpya ambao umebadilisha maisha, na fikra za binadamu.

Mbinu hii inapotumiwa katika fasihi huwa imetumiwa kimaksudi ili kudhihirisha jambo fulani. Mbinu ya ukiushi ina historia ndefu katika utunzi wa fasihi. Wananadharia na wanafasihi wamekiri, kwa mfano, kwamba mbinu ya ukiushi haiwezi kuepukika katika utunzi wa ushairi. Tangu awali, matumizi ya mbinu hii ya ukiushi yameelekea kusisitiza wazo kwamba, mbinu hii hutumiwa kwa malengo mawili: kiujumi na kudhihirisha maana katika fasihi. George Steiner (1976:217-218), kwa mfano, anasema, "Lugha ndicho kifaa muhimu ambacho binadamu anaweza kutumia kukataa kuuona ulimwengu jinsi ulivyo". Anachosisitiza katika madai haya ni kwamba lugha hutumiwa kukiuka maana ya kawaida na kuvumbua njia mpya za kuuona ulimwengu.

Dhana ya ukiushi katika fasihi iliasisiwa na mwanamaumbo mrusi Viktor Shklovsky ambaye aliunda dhana ya Kirusi 'Ostranenie' ambayo ilitafsiriwa katika Kiingereza kama "kueleza kwa njia ya ajabu" (making strange). Aliamini kwamba jukumu la fasihi lilikuwa kueleza au kubainisha ulimwengu kwa njia isiyokuwa ya kawaida. Alikiri kwamba jukumu la fasihi

lilikuwa kuchochea hisia za msomaji. Kwake 'Ostranenie' ilijumlisha mbinu zote ambazo mwandishi wa fasihi anaweza kutumia ili kubainisha kitu cha kawaida kwa njia ya kukifanya kieleweke kwa njia mpya. Kwa hivyo, alichukulia kwamba mbinu za ukiushi zililenga sio tu kudhihirisha maana, bali pia kutoa picha ya kipekee ya kile ambacho kilikuwa kikielezwa (Shklovsky 1965).

Mbinu hizi zinapotumiwa katika fasihi, hutufanya kuona mambo kwa njia iliyo tofauti kabisa na jinsi tunavyoyajua. Mbinu za ukiushi ni muhimu kwa sababu msomaji wa fasihi huzitambua moja kwa moja anaposoma. Anapokutana na mbinu hizi, yeye hulazimishwa kuzifikiria na kisha kutambua ile maana mpya inayokusudiwa na mwandishi.

Mbinu hizi ni nyingi na huweza kuwa za kitamathali kama vile jazanda, taswira, tashihisi, tashbihi na methali. Makala hii inafafanua jinsi Euphrase Kezilahabi na Said Ahmed Mohamed wanavyoshughulikia na kubainisha itikadi ya kuumeni (patriarchal ideology) kupitia mbinu za ukiushi. Watafiti wengi wameshughulikia mbinu mbalimbali za fasihi lakini si wengi ambao wamejaribu kuonyesha jinsi uhakiki wa mbinu za ukiushi unavyoweza kutumiwa kuelewa maana katika kazi za fasihi. Msimamo wetu ni kwamba mbinu za ukiushi ni muhimu katika utunzi wa fasihi na uchunguzi wa mbinu hizi unaweza kubainisha maudhui ya mwandishi kwa njia nzuri zaidi.

## Nadharia

Kama tulivyotaja hapo juu, dhana ya ukiushi ina misingi yake katika nadharia ya fasihi ya umaumbo (formalism). Wanamaumbo walilenga kuchunguza sifa tambulishi za maandishi ya fasihi. Katika uchunguzi wao, walichukulia fasihi kama tukio la kiisimu. Kwa mfano, walichukulia kwamba kazi ya mshairi ilielezwa kuwa ya kufinyanga lugha wala sio kuelezea uhalisi uliokuwepo katika jamii . Kwa sababu ya msimamo huu, walihakiki ushairi kwa kuorodhesha mbinu mbalimbali za matumizi ya lugha bila kuhusisha matumizi haya na hali halisi ya maisha ya jamii. Kwa mfano, itikadi haikuhusishwa hata kidogo.

Makala hii inachukua msimamo kwamba kazi ya fasihi ni zao la kijamii na lazima ihakikiwe katika msingi na muktadha wa jamii husika. Kwa hivyo, katika uchambuzi wetu wa mbinu za ukiushi tunatambua umuhimu wa matukio ya kijamii katika kuelewa maana ya mbinu hizi. Tunashikilia kwamba miktadha ya kiitikadi, kijamii, kitamaduni, na kihistoria huchangia

katika uelewa wa kazi ya fasihi. Mwandishi wa fasihi hueleza hisia na itikadi zake za kibinafsi na falsafa za jamii yake.

Kwa hivyo, nadharia iliyotumika ni ya uhakiki makala (Critical Discourse Analysis Theory – CDA). Nadharia hii ina waasisi wengi wakiwemo; Fowler, Fairclough, van Dijk na Wodak. Wote wanasisitiza kwamba matumizi ya lugha ni kitendo cha kijamii (social discourse). Kijumla nadharia ya CDA ina mihili ifuatayo kwa mujibu wa Wodak & Meyer (2001):

(i) Matumizi yoyote ya lugha ni tukio la kijamii.

(ii) Katika uhakiki wa makala, nadharia hii huchunguza miundo ya makala kwa kurejelea sifa zake za kiisimu pamoja na vipengele vya kijamii na utamaduni. Inashikilia kwamba maana kamili ya makala hudhihirika kupitia ushirika wa vipengele hivi viwili.

(iii) Inashikilia kwamba uhusiano baina ya wanajamii huathiri na kudhihirika kupitia kwa jinsi wanajamii hawa wanavyozungumza baina yao na kujieleza.

(iv) Ni nadharia ya kisasa ambayo haitoi msimamo maalum juu ya maswala ya ulimwengu. Kwa hivyo, inachukulia kwamba uhakiki wowote ule na matokeo yake yachukuliwe tu kama mojawapo ya jinsi ya kuelewa swala fulani.

(v) Inalenga kutoa mitazamo mbalimbali kuhusu maswala yanayohusu jamii.

(vi) Nadharia hii huchunguza dhana, mifumo ya kiitikadi, maadili na misimamo ya kijamii kwa lengo la kuielewa upya.

Kijumla, kwa kutumia nadharia hii, makala inashikilia kwamba matumizi yoyote ya lugha yanaelekezwa kwa misingi na mipaka ya mfumo wa kijamii na kitamaduni. Kwa hivyo, katika uhakiki wetu tunajaribu kuonyesha uhusiano baina ya uteuzi wa mbinu za ukiushi za waandishi hawa na miktadha yao ya kijamii na kitamaduni, pamoja na mifumo ya kiitikadi.

## Mfumo wa kuumeni

Mfumo wa kuumeni unaweza kufafanuliwa kama itikadi katika utaratibu wa jamii ambapo huendeleza na kumpa mwanamme nafasi ya juu kuliko mwanamke (Masinjila 1994:1). Mfumo huu humpa mwanamume uwezo na mamlaka kuhusu uzazi, kazi na hata urazini dhidi ya mwanamke. Chanzo

cha itikadi hii kinapatikana katika asasi mbalimbali za kijamii ambazo h
mikakati ya amali, shughuli za kijamii na tabia au mielekeo mbalimbali ya kijamii kwa kuzingatia maoni ya wanaume. Kwa mfano, katika jamii nyingi za Kiafrika, baba (mwanamume) ndiye kinara wa asasi ya familia. Ikiwa hayupo kutoa mwelekeo kuhusu maswala fulani, watoto wake wa kiume ndio wanaochukua nafasi hiyo hasa kutoa mwelekeo kuhusu ndoa, elimu na kadhalika. Itikadi hii ina historia ndefu ambayo imejikita katika tamaduni za jadi. Tamaduni hizi zimechukulia maoni na fikra za wanaume kuwa ndiyo msimamo wa jamii kwa jumla.

Kupitia mfumo huu, itikadi nyingi za kijamii na kitamaduni husisitiza hali ya kumbainisha mwanamume kama kiumbe bora kuliko mwanamke. Itikadi hizi huelekea kusisitiza kwamba mwanamume ni bora zaidi kihulka na mwanamke ni kiumbe dhaifu ambacho hakina jingine la kufanya ila kutegemea mwanamume kwa kila hali. Katika kuimarisha mwelekeo huu, jamii huweka mikakati imara kupitia asasi mbalimbali za kijamii ambazo zinaendeleza mawazo, imani na mila ambazo huidhinisha na kuhakikisha kwamba hali hii haibadiliki bali inahifadhiwa kwa vyovyote vile.

Fasihi kama mojawapo ya njia za kupitisha amali, imani na mila za jamii imetumiwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kuendeleza lengo hili. Hata hivyo, baadhi ya riwaya tulizoshughulikia zinaelekea kupinga baadhi ya misimamo, itikadi na mila hasi zinazombainisha mwanamke kupitia macho ya itikadi hii inayoendelezwa na mfumo wa kuumeni.

## Mifano ya ukiushi

1. Mfumo wa kuumeni unapingwa vikali na Mohamed katika riwaya ya *Asali Chungu* kupitia jazanda.

   > Mzee Omari alipokwisha kuondoka, Zuberi jicho lake likapiga kwa mboga utashi wake mpya. Hivyo akajidhihirisha 'funza anayerukia viale vya majani machanga na kuviangamiza (Mohamed 1977:21).

   Mohamed anapinga ndoa za kupanga kupitia jazanda ya funza kwa kuwabainisha wazee wanaowaoa wasichana wachanga kama Mboga kuwa waangamizaji. Katika jazanda hii viale vya majani machanga ni Mboga ambaye hajakomaa kuanza majukumu ya ndoa. Taswira ya funza kuangamiza majani machanga inasisitiza msimamo wa mwandishi kwamba wazee kama hawa ni waharibifu.

2. Mohamed anasisitiza msimamo huu pia kupitia *Dunia Mti Mkavu* (1980:26) ambapo msichana mchanga ameshaozwa na anamtuma dada yake kumpelekea mchumba wake wa halali ripoti kwamba ameozwa na babaye bila hiari yake. "Amesema dada umsamehe, ameshaolewa kwa nguvu. Ameuzwa na baba..."

   Maanaya matamshi haya inabainika kupitia kitenzi 'ameuzwa' kinachodhihirisha kwamba babake Kazija amekubali kutoa bintiye kwa ndoa ili apate faida ya kifedha. Mtoto wa kike anabainishwa kama mali ya babaye ambaye anaweza kumwoza kwa yeyote aliye na uwezo wa malia au wa kifedha unaomridhisha .

3. Mohamed katika *Asali Chungu* analalamikia matarajio ya jamii kuhusu mwanamume katika familia. Shaaban na Dude hawajaoa na Shaaban anapomuomba Dude kuoa anamjibu:

   > Ama kweli ulikuwa ukiota! Mimi nikataka mke? Mimi mwenyewe ningalipaswa kuolewa ikiwa ni kuowa, wa kuowa ni wewe Mzee Shaaban" (Mohamed 1977:33)

   Dude hawezi kuoa kwa sababu hana kazi ya kumwezesha kutimizia familia na kwake afadhali Shaaban aoe kwani ana biashara ya kuuza supu. Katika utamaduni wa Waswahili mwanamume huoa na mwanamke huolewa. Katika ndoa mwanamume ana mamlaka dhidi ya mwanamke kwa sababu yeye ndiye ameoa. Lakini Mohamed anakiuka hali hii ya kawaida wakati Dude (mume) anaposema kwamba afadhali aolewe. Kupitia ukiushi huu Mohamed anaonekana kupinga msimamo wa jamii juu ya kazi zinazotengewa jinsia mbalimbali. Matumizi haya ya kinaya yanaelekea kupinga itikadi inayosababishwa na mfumo wa kuumeni inayomfanya mwanamume kukosa mke kwa sababu hana njia ya kukimu jamii yake. Maoni yetu ni kwamba ukiushi huu unatufanya kufikiria zaidi kuhusu hali halisi ya jamii ambapo kuna uwezekano wa mke kuwa na uwezo wa kukimu jamii hata kama mume hafanyi kazi yoyote.

4. Mohamed katika riwaya hiyo pia anaonyesha jinsi jamii inavyobebesha wanaume mizigo mingi inayokuja pamoja na mfumo wa kuumeni. Omari anamlalamikia Zuberi kwamba asimwondoe shambani kwa sababu ya mizigo mingi aliyo nayo ya kukimu jamii yake.

> Tafadhali bwana angu! Usinione mimi, ila waone walio mgongoni pangu. Nikitoa mazao yangu yote niliyopanda matumbo manane nitayalisha nini mimi? (Mohamed 1977:18-19).

Ingawa jazanda iliyotumiwa ya matumbo manane inadhihirisha ukatili wa Zuberi, inabainisha fikra za itikadi ya kuumeni kwamba mwanamume ndiye anayestahili kutimizia jamii yake mahitaji yote. Yaani mkewe na watoto wanastahili kula jasho lake.

5. Mohamed katika *utengano* anadhihirisha nafasi ya mwanamke katika jamii, ili kuonyesha jinsi jamii inavyoratibu mahusiano baina ya jinsia. Jambo hili linadhihirishwa kupitia majibizano baina ya maksuudi na Biti Kocho.

> Mwanamke huyu anataka nini? Mbona anakuja kwa meno ya juu. Sasa ameshaingia bahari nyingine na mazungumzo yake kuyaelekeza pabaya. Wanawake kama hawa wameenea siku hizi ... Wanajuaje siasa hawa wajinga, watu. Eee katafute kifuu na mchanga uchezee (Mohamed 1980:51).

Maksuudi haamini kwamba anaweza kujibizana na mwanamke wakati anamtia adabu mkewe. Inaonekana anakubali kwamba kuna kizazi kipya cha wanawake wa tabia kama za Biti Kocho ambao, wanajaribu kujibizana na wanaume lakini kwake wanawake ni wajinga. Itikadi ya kuumeni na taasubi ya kiume ndiyo chanzo cha fikra za Maksuudi. Kwa sababu hii, anamkumbusha Biti Kocho nafasi yake katika jamii ambayo siyo tofauti na ya mtoto. Utamaduni wa Waswahili huwataka watoto kuwa na heshima mbele za watu wazima. (Harris 1965; Salim 1978). Maksuudi anamhitaji Biti Kocho kudhihirisha heshima hii au "katafute kifuu na mchanga uchezee". Kupitia kejeli hii ambapo Maksuudi anamsihi Biti Kocho kucheza mchezo wa kitoto, Maksuudi anakiri kwamba hawawezi kujibizana kwani Kocho (mwanamke) ni kama mtoto na iwapo hana cha kufanya basi aende kucheza mchezo wa kitoto.

6. Kezilahabi anadhihirisha nafasi hiyo katika *Gamba la Nyoka*. Chilongo amelazwa hospitalini na anamwamrisha muuguzi kumhudumia, lakini muuguzi huyo anamwambia bado anashughulikia mgonjwa mwingine. Jibu hili linamkera na anajibu:

> Funga domo lako! Ninao wanne nyumbani! Hawasemi neno nikikohoa! (Kezilahabi 1970:53).

Chilongo hataji wake kwa jina na anakiri hawasemi akikohoa. Kwake mwanamke yeyote hatakiwi kujibizana na mwanamume bali kukubali tu anayoyasema.Ingawa matamshi haya yanadhihirisha itikadi ya kuumeni,kwa njia nyingine yanabainisha taasubi ya kiume.

7. Katika jamii nyingi za Kiafrika,jukumu la mwanamke muhimu ni kuzaa watoto wengi. Mohamed anadhihirisha hali hii katika *Utengano* ambapo Kazija analalamika:

    Nani kasema utumwa umeondoka?
    Viumbe vya kupika na kupakua
    kufua na kupiga pasi, kushika mimba na kuzaa,
    kuzaa, kuzaa kuzaa kama panya (Mohamed 1980:7).

   Ukiushi unadhihirika kupitia upangaji wa maneno kishairi, takriri na tashbihi; 'kuzaa kama panya'. Malalamishi ya Kazija yanadhihirisha majukumu mbalimbali ya mwanamke kama kupika kufua na kupiga pasi.Hata hivyo anasisitiza kuzaa kupitia kurudia neon "kuzaa" kasha kufananisha kuzaa na uzazi wa panya.Panya huzaa watoto wengi tena baada ya muda mfupi. Kurudia neno 'kuzaa' kunabainisha ukweli kwamba mwanamke anatarajia kuzaa watoto wengi bila kupumzika. Hili linamaanisha kwamba mwanamke ana kazi ngumu ya kuzaa na kulea watoto wengi kando na majukumu mengine ya nyumba.

8. Watoto wa kike ni hasara na taabu na mwanamke huheshimiwa katika ndoa iwapo amezaa mtoto wa kiume.Hili linatokana na itikadi kwamba mtoto wa kiume alichukuliwa kuwa na manufaa makubwa kwa kuendeleza ukoo kupitia kizazi kipya. Kezilahabi amebainisha hili kupitia *Rosa Mistika*. Ingawa Regina alizaa watoto wengi bado hakufurahisha mumewe kwani alitaka amzalie watoto wa kiume:

    Zakaria hakuwajibu lolote. Regina na Rosa walikuwa wamenyamaza tu. Mshenzi unanizalia wasichana tu! Unaniletea taabu nyumbani bure (Kezilahabi 1971:23).

   Ni ajabu kwamba Zakaria anaona watoto wa kike wanamletea taabu. Kwake Regina mkewe ni mjinga kwani hajamzalia mtoto wa kiume. Kwingineko, Zakaria analalamikia wageni wengi wanaomtembelea kwa sababu ya kuwa na wasichana.

    Kuzaa wasichana taabu sana!
    Unapata wageni wa kila aina. Kweli wasichana

> Watano walikuwa wengi na vijana sasa walizoea
> Kuita mji wake 'zoo'. (Kezilahabi 1971:38)

Mji wa Zakaria unaitwa kijazanda 'zoo'. 'Zoo' ni neno la Kiingereza linalomaanisha mahali wanyama wanatazamwa na kuuzwa.Matumizi yake katika muktadha huu yanamaanisha mabinti wa Zakaria wanafananishwa na vifaa vya kutamaniwa na vya kuvutia watu labda waweze kuvinunua. "Zoo" ni mahali ambapo wanyama hao huwa wamefungiwa pasipo na kutoka wala mtu kuingia bila ruhusa. Jazanda hiyo inaelekea kumaanisha kwamba wasichana ni dhaifu na wanahitaji ulinzi. Mwandishi anatumia taasubi ya Zakaria kubainisha itikadi ya kuumeni.

9. Katika *Kichwamaji*, Kezilahabi anarejelea wasichana kwa kuwataja kama 'matunda'. Fungameza anajaribu kumkataza Kazimoto asimuoe Sabina. Anaeleza:

> Sabina-nikwambie mtoto wangu – ni tunda baya na nisingependa wewe ulile (Kezilahabi 1974:161).

Jazanda ya kulinganisha mwanamke na tunda inampa mwanamke sifa za urembo, utamu, nyororo na sura ya kuvutia. Mwanamume anahitajika kudhihirisha tamaa yake kwa kula au kutafuna na kufurahia ladha yake.Kwa njia hii mwanamke anabainishwa kama kifaa cha kumfurahisha mwanamume na "kuliwa."

10. Jazanda hiyo ya kula inarejelewa tena katika *Asali Chungu*. Dude ameshiriki kitendo cha ngono na Amina na pia anapanga kumtembelea Amina kwa ajili ya kumposa bintiye Shemsa. Dude ana wasiwasi na mwandishi anaeleza wasiwasi yake hivi:

> Atakuwa vipi Bi. Amina atakapomwona amerejea, na katika kurejea huko anakwenda kumposa mwanawe Shemsa? Hata yeye mwenyewe Dude aliona vibaya. Inauma kufikiria kuwa hatimaye itambidi kula kuku na vifaranga (Mohamed 1977:143)

Mwandishi anafananisha kitendo cha Dude na "kula kuku na vifaranga" kumaanisha kwamba ni jambo lisilokubalika. Mwandishi anatumia taswira ya kula kuzungumzia kitendo cha ngono ambapo mlaji ni mwanamume ilhali kinacholiwa ni mwanamke.Hali hii inayoonyesha uhusiano kati ya mwanamke na mwanamume katika mambo ya ngono kinadhihirisha itikadi ya kuumeni.

11. Kezilahabi halikadhalika katika *Kichwamaji* anabainisha itikadi hiyo ya kuumeni kuhusu maswala ya ngono ambapo mwanamume ana uhuru wa kufanya mapenzi na wanawake wengi bila kunyoshewa kidole cha lawama. Kwa upande mwingine, mwanamke anayedhihirisha tabia hiyo anadharauliwa. Ni ajabu kwamba hata wanawake katika jamii wamekubali msimamo huo wa jamii bila kuupinga. Nyabuso aliyekuwa kahaba hapendezwi na Kazimoto kwa sababu ya kutodhihirisha sifa hii jinsi alivyotarajia. Anasema:"Kazimoto, jina bure lakini moto hauwaki "(Kezilahabi 1974:64).

Katika muktadha huu, neno 'moto' limetumiwa kijazanda kwa maana ya nguvu za kiume. Kutokana na jina la Kazimoto, Nyabuso alikuwa na matarajio makuu ambayo hayakutimika. Naye Kazimoto analaumu pombe. Kwa mujibu wa Tong (1989: 49) mfumo wa kuumeni humpa mwanamume uhuru katika mambo ya ngono. Jambo hili ndilo limesababisha mpangilio wa kijamii ambapo mume hukubaliwa kuoa wake wengi. Kezilahabi anadhihirisha hili kupitia Nyabuso. Anaeleza;

> Hajapata wachumba. Nani ataoa makapi? Huyo sasa amekuwa mpira wa kudunda na kuacha hapo wengine pia wadunde (Kezilahabi 1974:62).

Katika matamshi haya kahaba wa kike kama Nyabuso anatajwa kijazanda kama 'makapi' na 'mpira wa kudunda'. Makapi ni uchafu unaotolewa kutoka kwa nafaka na hutolewa kwa upepo. Jazanda ya makapi inambainisha kahaba wa kike kama mwanamke ambaye uzuri/utamu wake wote umeondolewa. Kahaba huyu hawezi kuchukuliwa katika ndoa bali ni wa kutumiwa tu na mwanamume yeyote anayetaka kujifurahisha. Kupitia jazanda hii, mwanamke kahaba anabainishwa kama kifaa cha kumfurahisha mwanamume.Hii hapa mifano mingine kutoka *Utengano*;

(i) "Alijibu Maimuna kwa hasira. Wewe ndiye unayenijua zaidi, na kama si wewe, ningalikwishatokomea zamani. Sirudi bibi, na hasa sasa. Nimeshakuwa *debe bovu*, sina la kukalia." (Mohamed 1980:83). Maimuna ambaye ni kahaba anajichukulia kama debe bovu ambalo mara nyingi halina manufaa kwani haliwezi kubeba maji.

(ii) "Maimuna alijikuta amelengwa kama *pakacha bovu* jaani. Na babake ati alikwenda kumtafuta kule Rumbalola. Wa nini tena Maimuna?

Ameshakuwa *kinyesi*" (Mohamed 1980:137). Katika matamshi haya Maimuna anajilinganisha na pakacha bovu na kinyesi. Kwa sababu ya kushiriki katika ukahaba anajiona kama ambaye hana manufaa yoyote.

## Hitimisho

Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi wamefaulu katika kutumia mbinu za ukiushi kubainisha itikadi ya kuumeni katika jamii. Imedhihirika kwamba mbinu za ukiushi zinaweza tu kueleweka ikiwa zitahakikiwa katika misingi na mipaka ya mifumo ya kijamii na kitamaduni. Pia makala hii imebainisha kwamba mifumo hiyo ya kijamii na kitamaduni huathiri uteuzi wa mbinu za ukiushi za waandishi wa fasihi. Hata hivyo, waandishi hawa wanaweza kupinga misimamo hiyo ya kiitikadi au wakaibainisha jinsi ilivyo.

## Marejeleo


Dijk, T.A.V. 1976. *Pragmatics of Language and Literatue*. Amsterdam: North-Holland Publishing Company.

______. 1977. *Text and Context, Explorations in the Semantic and Pragmatics of Discourse*. London: Longman.

Fairclough, N. 1989. *Language and Power*. London: Longman.

______. 1995. *Critical Discourse Analysis: The Critical Study of Language*. London: Longman.

Fairclough, N. & R.Wodak. 1997. 'Critical Discourse Analysis' in Dijk, T.V. (ed). *Discourse Studies: A Multidisciplinary Introduction*, Vol. 2, London.

Fowler, R. (ed) 1975. *Style and Structure in Literature*. Oxford: Basil Blackwell.

______. 1971. *The Language of Literatue: Some Longuistic Contributions to Criticism*. London: Routledge and Kegan Paul.

______. 1966. Essays on Style and Language: A Linguistic and Critical Approach to Literary Style. London: Routledge and Kegan Paul.

Harriss, W.V. 1992. *Dictionary of Concepts in Literary Criticism and Theory*. New York: Greenwood Press.

Kezilahabi, E. 1971. *Rosa Mistika*. Nairobi: E.A.L.B.

______. 1974. *Kichwamaji*. Dar es Salaam: E.A.L.B.

______. 1978. *Gamba la Nyoka*. Nairobi: E.A.L.B.

Kress, G. and R. Hodge. 1979. *Language and Ideology*. London: Routledge & Kegan Paul.

Kress, G. 1989. 'History and Language: Towards a Social Account of Linguistic Change'. *Journal of Pragmatics* 13 (3).

Masinjila, M. 1994. "Patriarchy' in Kabira et.al. (1994). Delusions, Essays on Social Construction of Gender, African Women Development and Communication Network, Nairobi.

Mohamed, S.A. 1980. *Dunia Mti Mkavu*. Nairobi: Longman.

______. 1980. *Utengano*. Nairobi: Longhorn.

______. (1977). *Asali Chungu*. Nairobi: East Africa Educational Publishers.

Salim, I.A. 1973. *Swahili Speaking Peoples of the Kenya's Coast*. Nairobi: East African Publishing House.

______. 1978. *People of the Coast*. London: Evans Brothers.

Shklovsky, V. 1965. "Art as Technique" in L.T. Lemon & Reis, M.J. (edit. & trans.) *Russian Formalists Criticism*: four essays. Loncoln: University of Nebraska Press (Original Work Published in 1917).

Stacy, R.H. 1977. *Defamiliarization in Language and Literature*. U.S.A.: Scherkman Publishing Co.

Steiner, G. 1982. (ed) *The Prague School, Selected Writings 1929-1946*. Texas: Austin.

Tong, R. 1989. *Feminist Thought*. Colorado: Westview Press.

Wodak, R. 1989. 'Introduction' in Wodak, R. (ed) *Language, Power and Ideology.* Amsterdam: Benjamins.

Wodak, R. & C. Ludwig. (eds) 1999. *Challenges in a Changing World: Issues in Critical Discourse Analysis*. Vienna: Passagenverlag.

Wodak, R. and M. Meyer. 2001. (eds) *Methods of Critical Discourse Analysis.* London: Sage Publications.